turathi zisizogusika

United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

2005 60 1945

TOLEO LA MESSENGER LA TURATHI ZISIZOGUSIKA

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA
www.unesco.org/culture/ich





APRILI 2006 nº 2
ISSN 2071-7784

## Hali ya Kuidhinishwa

Kuidhinishwa na Mataifa Wanachama kufikia Machi 31, 2006

1 ALGERIA
2 MAURITIUS
3 UJAPANI
4 GABON
5 PANAMA
6 UCHINA
7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
8 LATVIA
9 LITHUANIA
10 BELARUS
11 JAMHURI YA KOREA
12 USHELISHELI
13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
15 MALI
16 MONGOLIA
17 CROATIA
18 MISRI
19 OMANI
20 DOMINICA
21 HINDI
22 VIET NAM
23 PERU
24 PAKISTANI
25 BHUTAN
26 NIGERIA
27 ICELAND
28 MEXICO
29 SENEGAL
30 ROMANIA
31 ESTONIA
32 LUXEMBOURG
33 NICARAGUA
34 CYPRUS
35 UHABESHI
36 BOLIVIA
37 BRAZIL
38 BULGARIA
39 HUNGARY
40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
41 JAMHURI YA MOLDOVA
42 YORDANI
43 SLOVAKIA
44 UBELGIJI
45 UTURUKI
46 BUKINI

KATIKA TOLEO HILI

Mtazamo wa Maafikiano uk. 2
Nyanjani – Colombia uk. 3
Kalenda uk. 4
Turathi-Hai uk. 4

# Kituo cha kwanza cha kimaeneo cha kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH) kitafunguliwa nchini Peru

### Mnamo Februari 22, 2006, UNESCO pamoja na Serikali ya Peru walitangaza kuundwa kwa CRESPIAL ili kuhudumu kama mfumo wa kituo cha kimaeneo ulimwenguni

Kufuatia maamuzi ya Kongamano Kuu la 33 mnamo Oktoba 2005, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO Bw. Koichiro Matsuura na Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi ya Peru, Bw. Oscar Maurtua de Romana walikutana Paris mnamo tarehe Februari 22, 2006 ili kutia sahihi mkataba wa kuunda 'CRESPIAL; kile Kituo cha Kimaeneo cha Kulinda Tamaduni za Turathi Zisizogusika za Latini Amerika. Kituo hicho kitaanza kufanya kazi wakati wa msimu wa kiangazi, na kitakuwa huko Cuzco, mji mkuu na wa kale wakati wa himaya ya Inca.

Malengo kamili ya 'CRESPIAL' ni kuyatangaza Maafikiano ya 2003 na kusimamia shughuli za 'ICH' katika mataifa ya Latini Amerika. Zaidi ya hayo, Kituo hicho cha kimaeneo kitaanzisha mtandao wa kubadilishana habari na kuwaleta pamoja wataalamu, asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali, huku pakiwa na msisitizo wa uwakilishi wa kijamii na ushirikiano wa dhati. 'CRESPIAL' pia itasaidia mataifa yanayoshiriki kwa kuwatayarishia mafunzo na shughuli za kuihamasisha jamii. Katika awamu hii ya kwanza, kituo hicho kitazingatia kuunda mtandao wa asasi za kimaeneo zilizojitolea kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika.

Serikali ya Peru tayari imetenga mchango maalum wa fedha takribani dola za Marekani 500,000 ili kusimamia kituo hicho. Bajeti hiyo itaongezewa michango ya mataifa mengine. Mataifa ya Latini Amerika yatakayotaka kujiunga na CRESPIAL, yatafanya hivyo kwa kuitaarifu rasmi UNESCO kupitia kwa njia zake rasmi za kitaifa. Mkutano wa kwanza wa mataifa yenye nia ya kujiunga utafanyika huko Brazil, hapo mwezi Mei (*tazama kalenda*).

Kituo hicho cha Cuzco kitahudumu kama mfano bora kwa masula mengine kama hayo katika maeneo mbali mbali ulimwenguni. Serikali ya Algeria na ile ya Korea tayari wameonyesha nia yao ya kufungua vituo kama hivyo vya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ICH), katika maeneo yao. Kwa habari zaidi wasiliana nasi kupitia wavuti wetu: www.crespial.org

## Tahariri

**Toleo la pili la *Messenger* limechapisha kwa uwazi orodha ya mataifa ambayo yameyakubali Maafikiano ya 2003 kufikia terehe 31, Machi 2006.**

**Tumefurahi kugundua ya kwamba tokea baada ya kuchapisha toleo lililopita, orodha hii ya mataifa wanachama imeongezeka kwa idadi ya mataifa 14, na kuifanya idadi kamili ya mataifa wanachama kuwa 46. Ama kwa kweli, hatukuyatarajia matokea haya. Hata hivyo, usawa wa maeneo ya kijiografia tayari umefikiwa: Mataifa 5 hadi 10, kila moja wapo likiwa linatoka kwenye makundi 6 ya kiuchaguzi ya UNESCO, yamepitisha Maafikiano hayo. Mataifa mengine 10 yanatarajiwa kujiunga na wenzao kabla Mkutano wa Kongamano kuu hapo Juni 27-29. Kulingana na kanuni za Maafikiano haya, Mataifa Wanachama kwa wakati huu yanatekeleza masharti ya makubaliano hayo.. Kwa kufanya hivyo, wanaboresha uanuwai wa tamaduni, ubunifu wa jamii mbali mbali na vikundi vya watu wanaoishi karibu na jamii hizo.**

**Toleo hili la *Messenger* limeangazia pakubwa kuhusu Latini Amerika na maeneo mengine yanayodumisha tamaduni zao za turathi-hai: Kuundwa kwa Kituo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika huko Peru, kampeini ya habari ya Colombia iliyofana sana, na kuanzisha miradi yenye mbinu za kiuvumbuzi inayoendelea huko Venezuela.**

***Rieks Smeets***
*Kitengo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika*



© Instituto Nacional de Cultura / Dante Villafuerte

***Taquille na usanii wake wa nguo.Kito kilichopatikana mnamo mwaka wa 2005. Wanaume, wanawake na watoto wa Kisiwa cha Taquille wakiwa katika Ziwa Titicaca, Peru, wakidhihirisha mila za kushona viroshi; hali iliyokuwa nyakati za watu wa Kihispania. Uuzaji wa nguo unachangia pakubwa katika ukuaji wa uchumi wa kawaida na maendeleo.***



Photos: © Margi Kathakali and Kutiyattam School



*Maonyesho ya Kutiyattam Sanskrit. Kito cha Thamani kilichotangazwa 2001. Maonyesho ya Kutiyattam yanayosifika kutokana na ishara za ajabu za uso yameendelea kudumu kama mila ya zamani sana nchini India. Mchanganyiko huu wa matini za Sanskrit* (kushoto) *na desturi za kiasili huigizwa katika mahekalu ya Wahindi, kusini kabisa mwa mkoa wa Kerala.*

**KANUNI YA 12 – rekodi ya vito vya thamani**

**1.** *Ili kuhakikisha kwamba turathi zimetambulika kwa urahisi kwa lengo la kuhifadhi, kila Taifa Mwanachama litatayarisha kwa namna yake, rekodi moja au zaidi ya turathi za tamaduni zisizogusika kwenye maeneo yake. Rekodi ya aina hii itakuwa ikibadilishwa na kuongezewa kila baada ya muda.*

**2.** *Baada ya kila Taifa Mwanachama kutoa ripoti yake kwa Kamati husika, kufuatia kifungu cha 29, litatoa habari kamili kuhusu rekodi hiyo ya vito vya thamani*

# Mtazamo wa Maafikiano hayo

## Wataalamu wanashughulikia suala la mbinu za kiuvumbuzi, jukumu kamili la Mataifa Wanachama

Kulingana na Kifungu cha 12 cha Maafikiano hayo, kila Taifa Mwanachama linahitajika kuunda na kusimamia “kwa njia ya kujilinda kivyake, ubunifu mmoja au zaidi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika zilizopo katika eneo lake”. Maneno kama haya yasiyo na misingi thabiti huyafanya baadhi ya Mataifa Wanachama kuchukua nafasi yao ya kutozishughulikia mbinu za kiuvumbuzi, isipokuwa uchunguzi wa karibu kuhusu Maafikiano hayo unaonyesha kwamba, kuna jinsi ambavyo Mataifa Wanachama wanavyoweza kupata nafasi ya kuchagua namna yatakavyotekeleza majukumu yao.

Katika harakati ya kuyajibu maswali ya mbinu za kiuvumbuzi yaliyotumwa na baadhi ya wahusika wa Mataifa Wanachama, UNESCO iliitisha mkutano wa wataalamu mnamo mwezi Machi mwaka wa 2005. Kulingana na ripoti ya mkutano huo, (inayopatikana kwenye wavuti), Kitengo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika, kinatayarisha ukurasa wa wavuti wetu wenye maelezo muafaka kuhusu uvumbuzi au ubunifu, ambao pia utatoa mielekeo mbali mbali katika mataifa mengine husika.

Inafaa ikumbukwe kwamba huu uvumbuzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika, kama inavyoelezwa kwenye Maafikiano, huhudumia kitu maalum; “kuhakikisha kujieleza kwa lengo la kulinda”. Kwa sababu neno ‘kulinda’ linamaanisha “kupima ili kuhakikisha usawa wa kitu”, basi linamaanisha kwamba, uvumbuzi huo unafaa kuingizwa kwenye orodha ya tamaduni-hai na kwamba ile taarifa kuhusu kuwezekana kwake ni muhimu ihusishwe.

Mbinu mojawapo iliyoundwa kitambo ni kuhusika kwa wanajamii na vikundi katika kutambulisha na kulinda Turathi zao za Tamaduni Zisizogusika. Kama ilivyo katika Kifungu cha 2, Turathi za Tamaduni Zisozogusika ni lazima zitambuliwe na jamii pamoja na vikundi kama tamaduni zilizo kwenye turathi zao za kitamaduni. Kwa hali hii, Kifungu cha 11 kinahitaji Mataifa Wanachama kutenga na kufafanua vipengee mbali mbali vya turathi za tamaduni zisizogusika zilizopo kwenye maeneo yao, kwa kuihusisha jamii, vikundi na mashirika maalum yasiyo ya kiserikali. Mkutano huo wa Machi 2005 ulisisitiza umuhimu wa kuhusishwa kwa jamii. Katika mkutano mwingine, wataalamu walipendekeza kuongeza kipengee kitakachounga mkono kuhusishwa kwa wanajamii ‘’kwa hoja zao huru za kimsingi”.

Uvumbuzi na Katalogi ya kitaifa iliyopo, iliyopatikana kupitia kwa asasi za kiutafiti na mawakala wa wizara, unatofautiana kimaandishi na kimtazamo. Baadhi ya asasi hizo zimepanga vito hivyo kupitia idara za kiusimamizi, huku asasi nyingine zikipanga turathi hizo kulingana na jamii ama viwambo (mf. Muziki, densi na maarifa ya ethnolojia na sayansi ya mimea). Kwa sababu Maafikiano hayatoi mfumo rasmi wa mpangilio wa kanuni zake, Mataifa Wanachama yana uhuru wa kupanga uvumbuzi au ubunifu wao kwa njia wanayoiona itayafaa mahitaji yao. Licha ya Mataifa Wanachama kuagizwa kuundwa kwa ‘’uvumbuzi mmoja au zaidi”, hali hii huimarisha mpangilio huo.

Wataalamu wanafahamu ya kwamba suala la kuwepo kwa uakibishaji wa uvumbuzi kamili litakuwa na matatizo mengi, hususan mataifa ambayo yamezongwa na tamaduni, mila na kuwepo kwa lugha nyingi. Uvumbuzi au ubunifu sio lazima uhusishe kuwepo kwa nyaraka nyingi, kwani lengo kamili ni kufahamisha na kutoa mwongozo bora, ili kuweza kuzifahamu faridi mbali mbali zinazohitaji kulindwa na kuhifadhiwa. Iligundulika kwamba, kupatikana kwa habari zaidi itabidi kuwekewe mikingamo ili kuheshimu haki-miliki za amali, ama, kama ilivyoelezewa katika Maafikiano, kuheshimu utendakazi wa tamaduni zinazolinda turathi za tamaduni zisizogusika. Kamati maalum kati ya serikali mbali mbali ilichaguliwa mwishoni mwa mwezi Juni 2006. Bila shaka ingependelea kutoa mapendekezo yake kuhusu suala hilo.

Katika mikutano miwili iliyofana, wataalamu walifafanua hojaji hiyo iliyokuwa na maswali 25 kwa kina. Chombo hiki ambacho ni rahisi kutumia kinaweza kutumiwa na mataifa ambayo hayana tajriba kwenye masuala ya kiuvumbuzi. Hojaji hiyo imeundwa ili kuwasilisha taarifa ya kutosha kwa kila faridi katika ukurasa mmoja. Nakala ya hojaji hii itapatikana kwenye wavuti wa turathi za tamaduni zisizogusika kufikia mwisho wa mwezi wa Aprili mwaka 2006.

## Utafiti: Venezuela inaendelea

Jaribio la kipekee linaendeshwa huko Venezuela. Mradi huu ulioanzishwa mwaka wa 2003, ulifahamika kama ‘’Tamaduni ya Censo del Patrimonio Venezolano” na tayari umepata usajili wa zaidi ya faridi 60,000 za turathi zenye mguso na zile zisizogusika kutoka kwa taifa zima la Venezuela. Kufikia mwisho wake hapo mwaka wa 2006, Rekodi hii inatarajiwa kuwa na zaidi ya turathi 100,000, na matokeo yake yatachapishwa kwenye zaidi ya vitabu 320, kila kitabu kikieleza wilaya maalum ya kiusimamizi. Data hiyo pia itapatikana kwenye SIDII-ROMU na kwenye Tovuti.

Rekodi iliyokusanywa kutoka katika hojaji, imegawanywa katika mafungu matatu (bidhaa, turathi iliyojengeka, miundo ya kibinafsi, mila za masimulizi na matukio ya pamoja). Kila turathi itahusisha ujumbe mfupi na picha. Utafiti huu wa Venezuela ulioanzishwa kabla ya kupitishwa kwa Maafikiano haya ya turathi za tamaduni zisizogusika, umeendelea kufuata kanuni na masharti ya Maafikiano hasa kwa kuuhusisha uwakilishi wa wanajamii. Mahakama Kuu ya Venezuela iliamuru kwamba rekodi na ubunifu wa aina yoyote ile utalindwa na sheria za nchi hiyo. Turathi za Kitamaduni zitapewa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba haziangamii.







Photos: © Fernando Mercado



*Juu na Kulia, Sherehe za baranquilla. Vito vya thamani vilivyotangazwa katika 2003. Shina la mila za kiasili za Waafrika na wazungu, sherehe ya kila mwaka inayofahamika zaidi huko Colombia hujumuisha mashabiki wengi, wakiwemo wanamuziki, wachezaji na wasanii.*

*Chini, bango la kutangaza sherehe za Ki-Clestrinye Ahellil kutoka Gourara.*

© ICANH




*Kito cha thamani kilichotangazwa mwaka wa 2005. Wa-Zenete kutoka Gourara wanaoishi kusini magharibi mwa Algeria ndio wamiliki wa kito cha Ahellil ambacho ni cha Ushairi unaochezwa na makundi makubwa ya wanamuziki, waimbaji na wachezaji kwenye sherehe mbali mbali.*

© CNRPAH 2004



# Nyanjani – Colombia

## Mamlaka ya UNESCO pamoja na ya Colombia yalipitisha kampeini ya miaka 3 ili kuhamasisha Wa-Colombia kuhusu turathi-hai

Kila mwaka huwa na zaidi ya sherehe 700 za kitamaduni na maadhimisho pamoja na takribani lahaja na lugha 67 ambazo zimekataa kufifishwa na watu, vita vya utumiaji silaha na hali ya uharibifu wa kimazingira. Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Colombia zimeorodheshwa kama zilizo bora kabisa katika majimbo ya Latini Amerika. Uanuwai huu si wa kushangaza mno ukizingatia idadi ya watu wa Colombia iliyo na makundi ya jamii 83 na yenye jamii ya watu wengi kutoka barani Afrika.

Kwa kuzingatia jukumu kamili la Turathi za Tamaduni Zisizogusika katika utangazaji wa ubunifu, usamehevu na amani, Kitengo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika cha UNESCO kiliamua kuchukua hatua kabambe ili kuisaidia Colombia kulinda Turathi zake Hai. Kufuatia udhamini wa Serikali ya Ujapani, mfadhili muhimu sana wa shughuli za kitengo hiki kutokea miaka ya 90', UNESCO na Serikali ya Colombia walizindua kampeni ya taifa zima katika mwaka wa 2002 ili kuwafahamisha wanajamii, mashirika ya umma, asasi za Kisayansi na Kiserikali kuhusu umuhimu wa kulinda Turathi Zisizogusika za Colombia.

Katika uendeshaji wa shughuli zake, mradi huu ulifanikiwa kufanya mambo yafuatayo:

- Uanzishaji wa Kamati ya Turathi Zisizogusika (2004), halmashauri ya Ushauri ambayo ni ya Wizara ya Tamaduni kuhusu uundaji wa sera na ufafanuzi wa vigezo vitakavyotumiwa kutayarisha orodha ya turathi.
- Kutangaza matangazo matatu kwenye Vituo vya Kitaifa na vile vya Kimaeneo vya Runinga, jumbe 40 kutangazwa katika vituo 200 vya kibiashara vya Redio na vituo vya kijamii. Kampeni ya matangazo katika magazeti makuu. Mikakati ya mawasiliano iliyokuwa na mada ''Onyesha Wewe ni Nani", ilipandisha hamasa kwa watu wengi, hususan kwa vijana wa Colombia, ili kudhibiti tamaduni za Wa-Colombia.
- Kupanga kuwepo kwa warsha tano za majanibu mbali mbali ili kuhimiza jamii, mawakala wa tamaduni, vikundi vya wanajamii na wataalamu wa kielimu na mawasiliano ili wajihusishe katika ulinzi huo wa turathi zao.
- Kupanga kuwepo kwa Mkutano wa Kwanza za Kitaifa wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika huko Medellin, (Septemba 2005), uliosababisha kuundwa kwa mitandao ya kitaifa na kuwapa moyo wanasiasa ili waunge mkono kuidhinishwa kwa Maafikiano hayo.
- Kuchapisha kabrasha ya kielimu na mwongozo utakaohusisha mbinu za kuwezesha kukusanya Turathi za Kwanza za Tamaduni Zisizogusika za Colombia (RIPIC). Kuunda kiakaba-data kitakachoweza kuambatanisha taratibu za kitaifa, kilichofanikisha majaribio ya miradi ya uvumbuzi wa turathi (muziki wa kitamaduni na densi ya Gran katika eneo la Magdalena).
- Kuunda Wavuti wa kusambaza mawasiliano ya kuhamasisha habari katika asasi, na taarifa nyinginezo muhimu (viunganishi, marejeleo ya kibibliografia, habari kuhusu rekodi za vito).

Lengo Kuu la Mradi lilikuwa ni – Hatua ya kuhusisha umma na wenyehisa katika hatua za ulinzi na kutafuta usaidizi wa kulinda turathi za tamaduni zisisogusika kutoka kwa waundasera na wahusika waliochaguliwa - hatimaye lilifanikiwa.

Tunashukuru sana kwa ushirikiano kati ya UNESCO na Serikali ya Colombia uliokuwa na ufanisi mkubwa. Hali ya kulinda turathi za tamaduni zisizogusika kwa wakati huu ni suala lenye umuhimu wa kitaifa na limepewa kipaumbele katika siasa. Colombia inakamilisha taratibu za maidhinisho hayo ya Maafikiano ya 2003.

Kwa habari zaidi wasiliana nasi kupitia:
www.patrimonioinmaterial.info

### MAELEZO YA MRADI

| | |
|---|---|
| JINA LA MRADI | Kampeni ya Kuuhamasisha Umma kuhusu umuhimu wa kulinda turathi zisizogusika za uzungumzaji huko Colombia |
| MCHANGIAJI | Hazina ya UNESCO/JAPAN ya Kuhifadhi na Kutangaza Turathi za Tamaduni Zisizogusika |
| BAJETI | Dola za Marekani 136,860 |
| MUDA | 2002–2005 |
| SHUGHULI | Uhamasishaji, kuelimisha, mbinu za uvumbuzi, kutangaza sheria za Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kitaifa. |
| ENEO | Colombia kote |
| ANWANI | Kitengo cha Turathi Zisizogusika, UNESCO, Paris<br>✦ César Moreno-Triana, c.moreno-triana@unesco.org<br>✦ Reiko Yoshida, r.yoshida@unesco.org |

MCHAPISHAJI Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)
Sekta ya Tamaduni, UNESCO
1 Rue Miollis
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa
Barua pepe: ich@unesco.org
Kipepesi: +33 (0) 145685752
MHARIRI MKUU Rieks Smeets
JOPO LA UHARIRI Estelle Blaschke, Fernando Brugman, Richard Lo Giudice, César Moreno-Triana, Ariana Morris, Reiko Yoshida
MWANA-RUWAZA Jean-Luc Thierry

***Tolea la Turathi za Tamaduni Zisizogusika*** linapatikana katika nakala zilizochapishwa na zile za kielektroniki katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

Matini yote inaweza kuopolewa katika wavuti (www.unesco.org/culture/ich) na kuchapishwa bila malipo ikiwa tu utataja shirika husika.



© Conselho das Aldeias Waiãpi-Apina

turathi zisizogusika

## KALENDA

MACHI 28 Sherehe ya Kutuzwa: Cheti cha UNESCO kinachotuza Nafasi ya Tamaduni za Gong (Kito cha 2005). Jiji la Pleiku, Viet Nam.

APRILI *(tarehe kamili itatangazwa)*
Mkutano wa Eneo-Dogo: Uzinduzi wa Mpango wa Utendakazi wa kulinda lugha, muziki na densi za Kigarifuna, huko Belize, Guatemala. Honduras na Nicaragua (Kito cha 2001). Belmopan, Belize.

APRILI 18 Sherehe ya Kutuzwa: Tuzo la Sheikh Zayed (UAE), wanatoa tuzo la vito viwili vya thamani vilivyopatikana mnamo 2005. UNESCO, Paris.

✦ **APRILI 20 Kuanzishwa kwa ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika.**

APRILI 20-21 Mkutano wa Wataalamu: ''Matukio ya Kupokea Vito vya Thamani vya Uzungumzaji na Turathi Zisizogusika za Kibinadamu". UNESCO, Paris.

MWISHONI MWA APRIL Jarida la *Courier la UNESCO* (la kimtandao): Masuala muhimu yametengewa Turathi za Tamaduni Zisizogusika.
Mawasiliano: www.unesco.org/courier

MEI 5-6 Kongamano: ''Siasa za Turathi za Tamaduni Zisizogusika", Kituo cha Masuala ya Kimataifa cha Weatherhead, Chuo Kikuu cha Harvard, Cambridge, Marekani.

MEI 16-19 *(tarehe kamili itatangazwa)*
Mkutano: Kituo cha Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika katika Latini Amerika (CRESPIAL). Brasilia, Brazil.

JUNI 27–29 Mkutano wa kwanza wa Kongamano Kuu la Mataifa Wanachama kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika. UNESCO, Paris.

SEPTEMBA *(tarehe na eneo la mkutano kuamuliwa na Jopo la Kongamano)*
Mkutano wa Kwanza wa Kamati maalum kati ya Serikali za mataifa Wanachama ili kulinda turathi za tamaduni zisizogusika.

Kwa mawasiliano zaidi, tufikie kupitia: ich@unesco.org

## HABARI ZA TURATHI-HAI

### Mkutano wa ACCU-UNESCO wa kuhusika kwa jamii na turathi za tamaduni zisizogusika

Kikundi cha wataalamu 20 kutoka mataifa 18 wanaoshughulikia suala la nidhamu, walikutana huko Tokyo (Ujapani) tarehe 13-15 Machi, 2006 ili kujadili kuhusika kwao katika kulinda turathi za tamaduni zisizogusika. Mkutano huo ulipangwa na Kitengo cha Turathi za Tamaduni Zisizogusika cha UNESCO na Kituo cha Tamaduni cha Asia/Pacific cha UNESCO (ACCU). Mradi huu ndio wa hivi karibuni zaidi katika mikutano ya wataalamu iliyoandaliwa na Idara hiyo kupitia kwa mada kama vile mbinu za uvumbuzi (Machi 2005), Vigezo vya uteuzi (Desemba 2005) na kuhifadhi nyaraka na kuakibisha (Januari 2006).

Kwa misingi ya Vifungu vya 2.1,11,12,13 na 15 vya Maafikiano, mijadala hiyo iliegemea sehemu tatu kuu: Ufafanuzi na Utambuzi wa Jamii na vikundi vya kijamii; kuhusika kwa jamii katika uvumbuzi wa turathi za tamaduni zisizogusika; kuhusika kwa jamii katika matayarisho ya uteuzi wa orodha wakilishi ya vito. Sehemu maalum ilitengewa ushirika wa kimataifa.

Baada ya mjadala wa kusisimua, washiriki walikubaliana kuhusu maelezo haya (*tazama chini*), ili kuidhinishwa na kamati ya baadae kati ya serikali mbali mbali. Pia waliunda mapendekezo yatakayosaidia Mataifa Wanachama katika mikakati ya kuweka rekodi za turathi za tamaduni zisizogusika kwa kuzihusisha jamii na vikundi vya kijamii. Miongozo pia ilipewa ufafanuzi zaidi hasa katika orodha wakilishi ya vito ya 'ICH'. Hususan, wataalamu hao walipendekeza kwamba, turathi zilizopendekezwa kuteuliwa ziondolewe kwenye uvumbuzi wa kitaifa kama ilivyotajwa kwenye kifungu cha 12 cha Maafikiano haya, na ihusishwe katika orodha (isiyo rasmi) ya wawakilishi wa kitaifa. Kwa kuufahamu umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika shughuli za turathi zisizogusika, wataalamu hao pia waliwaagiza 'ACCU' kuboresha mshikamano huo kupitia asasi na wataalam kutoka maeneo ya Asia/Pacific na kwingineko. Matini yote kuhusu mapendekezo ya mkutano huo yanaweza kupatikana katika wavuti wetu.

#### MAELEZO YALIYOPENDEKEZWA NA WATAALAMU WA 'ACCU-UNESCO'

1. **JAMII** ni mtandao wa watu ambao maisha yao na mshikamano wao unatokana na uhusiano wao wa kihistoria ulio na mashiko thabiti ya mafundisho, ama ushirikiano na turathi zao za tamaduni zisizogusika.

2. **VIKUNDI VYA KIJAMII** vinajumisha watu wa jamii hiyo na wengine kutoka nje ya jamii hiyo wanaoshirikiana kwa mambo kama vile ujuzi, tajriba, na elimu maalum, na kwa hivyo wanatekeleza shughuli maalum kwa wakati huu na wakati ujao, kuunda tena na / ama ubadilishanaji wa turathi za tamaduni zisizogusika kama, kwa mfano, wasimamizi wa kiutamaduni, wahusika ama washirika wao.

3. **WATU BINAFSI** ni wale walio kwenye jamii au kati ya jamii nyinginezo na wana ujuzi, elimu, tajriba ama hulka nyingine, na hivyo basi kutekeleza shughuli maalum zinazohitajika wakati huu na wakati ujao, kuunda tena na / ama ubadilishanaji wa turathi za tamaduni zisizogusika kama, kwa mfano, wasimamizi wa kiutamaduni, wahusika na pale inapowezekana, washirika wao.

© DPC



*Kito cha thamani kilichopatikana mnamo 2005 huko Kankurang. Kilipigwa rangi kwa kutumia rangi ya mboga za majani (kunde), kimevalishwa majani makavu na kuvishwa kinyago, turathi hii ya Kankurang ni kiumbe kilichohifadhiwa, kinachoendesha mila za jamii ya Mandinka kutoka Senegal na Gambia.*